JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA

SHULE YA SEKONDARI YA WA SICHANA,

Anwani ya Simu "MKUU WA SHULE".
Simu nambari: +25526 2605404 /0767677788 **SANDUKU LA POSTA 152,**
Nukushi nambari: +25526 2605404 **TABORA.**
Barua Pepe: taboragirls@gmail.com

KUMB. NA. JI/TGS/177/ …. **Tarehe 19/05/2021**

JINA LA MWANAFUNZI……
S.L.P……
……

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA WILAYA YA TABORA MKOA WA TABORA KIDATO CHA TANO MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha **Tano,** Tahasusi ya…… katika shule hii mwaka 2021. **Shule ya Sekondari ya Wasichana Tabora** ipo kusini mwa kituo cha mabasi na stesheni ya reli, umbali wa km.3 toka stesheni ya reli na km.4 toka kituo cha mabasi Tabora Mjini kuelekea Kipalapala. Shule Imepakana na Sekondari ya Tabora Boys.
Kutoka stesheni au Kituo cha Mabasi mjini unaweza kukodi 'taxi' kuja shuleni, nauli ni sh. 5,000/-, Aidha zipo Bajaji (pikipiki za mataili matatu) nauli ni Tsh 3000/=, **Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 05/07/2021,** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 03.07.2021. na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 18.07.2021

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

- **Mwanafunzi anatakiwa kuja na sare/ mahitaji yafuatayo:-**

(i) Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi yanayoishia kwenye kiwiko cha mikono na yasiyobana mwili.(Mashati ya mikono mirefu kwa wenye mahitaji maalumu (Wenye Ualbino)

(ii) Nguo za kuvaa ndani ya shati ambazo ni Sidiria au "vest" za rangi nyeupe au nyeusi, Haturuhusu uvaaji wa nguo zenye rangi tofauti na hizi.

(iii) Sketi ya bluu bahari iliyokooza yenye mshono wa linda box kubwa mbele na nyuma, na malinda mawili kushoto na mawili kulia. **Urefu wa sketi ni kufunika kiwiko cha miguu kwa wote (kitambaa kizito cha suti)** Unashauriwa kuja kununulia kitambaa cha sketi huku Tabora kuepuka mkanganyiko wa rangi.

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi pair 2 vyenye kamba, visigino vifupi. Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo.

(v) Jozi mbili za soksi nyeupe zisizo na mistari ya aina yoyote. (free size zinazofika magotini).

(vi) Wanafunzi wa Kiislamu: Nusu kanzu nyeupe mbili za kitambaa cha tetroni nzito na hijabu **(Juba)** nyeupe mbili, ndefu zinazofunika kifua zisizo na urembo wa aina yoyote na hijabu nyeusi ndefu kwa ajili ya kushindia.

(vii) **Kwa ajili ya michezo:** Bukta ya njano, Raba nyeupe, T-Shirt ya njano yenye kola ya duara, Isiwe na maandishi wala michoro ya rangi yoyote ile. na sketi ya njano mshono wa solo , kitambaa cha tetron.

(viii) Shamba dress **(Gauni**) mbili rangi ya Zambarau (Purple) kwa ajili ya kushindia ,urefu ni **kufunika kiwiko cha miguu** kwa dini zote, kwa wenye mahitaji maalumu (wenye ualbino) shamba dress iwe na mikono mirefu. **(kitambaa kizito cha suti)**

2.2 Madaftari 12 Dozen 1 (counter Book) quire 4, kalamu za risasi na za wino na Mkebe wa vifaa vya Hisabati (**Mathematical set), Calculator** pamoja na **dissection kit** kwa wanaosoma masomo ya Sayansi (**PCB na CBG).** na Hesabu pia Advanced Learners Dictionary kwa **Wanaosoma masomo ya sanaa (Art),**

2.3 Fedha ya matibabu/ **Bima ya afya NHIF (Gharama yake ni 50,400/= kwa mwaka), kwa wanafunzi wasio na kadi za bima ya afya, mzazi unatakiwa kulipia elfu hamsini na mia nne (50,400/=) taslimu kwa** ajili ya kutengenezewa kadi ya bima .Pesa hii inalipwa kila mwaka ili kuendelea kunufaika na huduma hii**. Godoro size 2.5"x6",** shuka 3 (mbili za pinki na moja nyeupe), mto, foronya ya pinki na Chandarua 4"x6" rangi nyeupe.

2.4 Mahitaji mengine ya kibinadamu:

(i) Tranka (sanduku la chuma)1 kwa ajili ya usalama wa vitu vyake.na kufuri imara kwa ajili ya kufungia tranka.

(ii) Vyombo vya chakula (sahani, kijiko, kikombe, bakuli na ndoo ya Plasiki kijiko)

(iii) Picha 4 passport size akiwa amevaa shati la shule (jeupe) na ziwe na "background"(kivuli) ya bluu nyuma.

(iv) Taulo(01) Vitenge au Kanga doti moja ambavyo atajifunga wakati wa kwenda kuoga.

(v) Tracksuit rangi ya dark (bluu nyeusi) Jozi moja yenye mistari myeupe pembeni (ambayo atavaa wakati wa kujisomea usiku).

(vi) Sweta la Light Bluu lililofumwa kwa uzi mzito wa kufumia.Masweta haya yana patikana madukani Tabora, hivyo unashauriwa kununua Tabora ili kuepuka kununua sweta lisilo sahihi.

(vii) Gereni la lita tano kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.

(viii) Tshirt ya shule rangi ya kijivu aina ya manga.

(ix) Viatu vya wazi (open shoes) kwa ajili ya kushindia.

KUMBUKA: Simu haziruhusiwi shuleni.

- **Mwanafunzi analazimika kuvaa vazi la shule wakati wote awapo shuleni, hivyo asije na nguo za nyumbani .**
- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi .Kwa mawasiliano Mwanafunzi awapo safarini, tumia simu ya dreva au konda au mtu yeyote unayemuamini aliye safari na mwanao safarini. Kwa shuleni tumia namba ya Mwalimu wa usafiri shuleni, Namba: 0621970123 (Elisante sadick) .Kwa mawasiliano zaidi piga 0756020660 (makamu mkuu wa shule)**

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi, Tekinolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais– TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
(c) Kuhudhuria vipindi vyote vya dini kwa mujibu wa ratiba ya shule.
(d) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
(e) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(f) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(g) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na;
(j) Kutunza mali za shule.

MUHIMU:

1. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa, ni marufuku mwanafunzi kulala au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa

2. Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa mama, baba, mlezi, kaka ama dada tu na siyo mtu mwingine. Taarifa za misiba ziletwe moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule siyo kwa mwanafunzi. Mwanafunzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.

3. Ni marufuku kuvaa kandambili wakati wa chakula Bwaloni, au mazingira yoyote ndani na nje ya shule isipokuwa bafuni wakati wa kuoga na bwenini.

4. Wageni wanaotambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja kwa muhula yaani (mara 2 kwa mwaka), siku moja kabla ya mahafali ya kidato cha sita na Nne kwa kuitwa na uongozi.

5. Likizo zote mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani, hataruhusiwa kwenda kwa ndugu (ubalozini) kipindi cha likizo.

- Mzazi unatakiwa kuandaa pesa ya nauli ya kuja likizo fupi (kipindi cha pasaka na septemba) na likizo ndefu, mwezi Juni na Desemba, na kuituma shuleni pindi tu itakapohitajika (utajulishwa)
- Mwanafunzi harusiwi kuwa na urembo wa aina yoyote kama vile heleni, bangili, mkufu na pete za aina yoyote ile.

- Shuleni haturuhusu kusuka nywele, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuja na nywele fupi na hasinyoe mtindo wa aina yoyote ile.

3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji .
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa .
8. Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kutoa mimba .
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. **Kuwa na simu ya mkononi shuleni au kumiliki kifaa chochote kinachohusiana na simu.**

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI

(i) Fomu ya kupimwa afya yake (Form for Medical Examination) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

(iv) Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

MICHANGO:

(i) Ada/karo ya shule: Weka kwenye akaunti Na. 51001100067, Jina la akaunti ni :Tabora Girls' Secondary School Revenue Collection –NMB Mihayo.

Na	Fedha kwa ajili ya	Kiasi kinachotakiwa
1	Ada/karo ya shule	Kwa mwaka ni **Sh.70,000/=** Au alete **Sh.35,000/=** kwa muhula
JUMLA		**70,000/=**

(ii) Michango mingine: Weka kwenye akaunti Na. 51002501537, Jina la akaunti ni :Tabora Girls' Secondary School, Duka , NMB – Mihayo Branch Tabora.

Na	Fedha kwa ajili ya/vifaa	Kiasi kinachotakiwa
1	Tahadhari	**Sh.5,000/=**(Hairudishwi)
2	Kitambulisho	**Sh.6,000/=**
3	Mchango wa dawati	**Sh.30,000/=**
4.	Ukarabati wa samani	**Sh.15,000/= (kwa mwaka)**
5.	Wapishi na Walizi	**Sh. 30,000/= (kwa mwaka)**
6.	Nembo ya shule	**Sh.2,000/= (kwa mwaka)**
7.	Huduma ya kwanza	**Sh. 10,000/= (kwa mwaka)**
8.	Taaluma	**Sh. 20,000/= (kwa mwaka)**
9.	Mahafari	**Sh. 10,000/=**
10.	Mtihani wa Mock kidato cha 5	**Sh. 20,000/=**
	JUMLA	**Tsh. 188,000/=**

Zingatia:

- **Lipa pesa yote Benki isipokuwa pesa ya bima ya afya tu Sh. 50,400/= kwani pesa taslimu haitapokelewa. Kisha toa nakala ya pay- in -slip (Risiti) kwa ajili yako na original njoo nayo shuleni.**
- **Epuka kuchanganya pesa zote kwenye akaunti moja, Zingatia maeelekezo yaliyotolewa hapo juu ili kuepusha usumbufu utakaojitokeza endapo utachanganya hela ya ada na michango kwenye akaunti moja.**

Njoo na vifaa vifuatavyo:-

1. Brushi ya kusugulia ndani ya tundu la choo yenye mpini mfupi, iwe imara isiyoweza kuchomoka kwenye mpini wake kirahisi – (01)
2. Fyekeo (01)
3. Ufagio wa ndani (soft bloom) wenye mpini mrefu – (01)
4. Mifagio ya nje imara ya chelewa yenye mpini mrefu – (02)
5. Ndoo tupu za lita 10- (02)

6. Result slip (njoo na orginal pia toa nakala moja)
7. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
8. Bando za karatasi nyeupe (ream paper 02)

MWL. LYDIA M. ELIUD
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA
S.L.P. 152
TABORA

FORM NO. 1

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENTS' OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants.

Pupil's full name……

Age/Years……Sex……

Blood found (red and White)…….

Stool examination:…….

Urinalysis:……..

Venereal Diseases test:……..

T.B. test:……

Eye Test:……

Ears:……

Chest:…….

Spleen:……

Abdomen:……..

Urine for Pregnant:……

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

……..

……..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature:……..

Designation:……..

Station:……..Date:……

Official Stamp: ……

FORM NO. 2
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA TABORA
HABARI ZA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI……..
2. KABILA……...
3. TAREHE YA KUZALIWA…….MWEZI…….MWAKA…….
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA…….
   MKOA WA……..
5. DINI……DHEHEBU…….....
6. JINA LA MZAZI/MLEZI……
   (Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI…….(KIJIJI)
   …….. (TARAFA)
   …… (WILAYA)
   …….. (MKOA)
   Na. ya simu ya mzazi/mlezi…….
8. KAZI YA BABA/MLEZI…….
9. KAZI YA MAMA/MLEZI……..
10. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).
    …….
    …….
    …….
11. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (matatu tu), anuani zao kamili na Namba zao za simu na picha zao za passport zibandikwe kwenye maboksi mbele ya jina la ndugu.

(a) Ndugu…….. Uhusiano……. ☐

…….. ☐
(b) Ndugu…….. Uhusiano…….

…….. ☐
(c) Ndugu…… Uhusiano……..

…… ☐
……

…… ……
SAINI YA MWANAFUNZI **SAINI YA MZAZI/MLEZI**

TAREHE:……. TAREHE:…….

FORM NO. 3

MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi……. (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Saini ya mwanafunzi…….

Tarehe……

Shahidi

Jina kamili……..

Saini…….

Tarehe……..

FORM NO. 4

A: AHADI YA MZAZI:

Mimi…… (jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa……..Kidato cha……. Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

Saini ya Mzazi/Mlezi…….

Anuani kamili…….

Simu:……

Tarehe:…….